# Matumizi ya Usambamba kama Nduni ya Kimtindo katika Kuibua Maudhui ya Dini katika Riwaya ya *Paradiso*

*Victor Kyomuhendo, Mosol Kandagor* na *Samuel M. Obuchi*
*Chuo Kikuu cha Moi*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza matumizi ya usambamba kama nduni ya kimtindo katika kuibua maudhui ya dini katika riwaya ya *Paradiso.* Tunachunguza miundo mbalimbali ya kiusambamba iliyotumika katika riwaya hiyo kuibua maudhui ya dini. Suala la dini ni la msingi katika jamii mbalimbali kwa vile dini imeshikamana na maisha ya kawaida ya wanajamii. Ndani ya mada ya jumla ya dini, riwaya hii inaangazia dhamira zinazoathiri jamii kama vile ufisadi na ujilimbikiziaji mali, ufungamano wa siasa na dini, pamoja na masuala ya kijinsia. Tulidondoa vifungu kutoka katika riwaya hiyo kwa mkono kwa sababu haipatikani kielektroniki. Data iliteuliwa kimaksudi kwa kulenga maudhui yanayohusu suala la dini. Katika ukusanyaji na uchambuzi wa data tumetumia Nadharia ya Uchimuzi. Orodha ya kategoria za kiisimu na kimtindo ya Leech na Short (2007) ilitumiwa kubainisha ngazi kuu za uchunguzi wa kimtindo. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba usambamba ni njia kuu aliyoitumia mwandishi kuibulia na kusisitizia maudhui kuhusu dini. Usambamba huu unajitokeza katika ngazi za virai na vishazi na unahusisha aina mbalimbali kama vile anafora, epifora, tanakuzi na mjalizo. Usambamba wa aina ya anafora ndio umedhihirika zaidi katika riwaya ya *Paradiso.* Makala haya yanapendekeza kwamba usambamba wa kisintaksia unafaa kuhusianishwa na usambamba wa kileksika katika kuzichambua kazi za kifasihi za Kiswahili kimtindo.**

**Maneno Muhimu:** *Dini, Mtindo, Paradiso, Uchimuzi, Usambamba*

## Utangulizi

Kuna mikabala mbalimbali ya kuzichanganulia kazi za fasihi, mkiwemo uhakiki wa kifasihi, uchanganuzi wa usemi na uhakiki wa kimtindo. Uhakiki huu huzingatia masuala mbalimbali. Kipacha na Jilala (2021) wanasema kwamba uchunguzi wa muundo wa lugha uliojenga matini ya kifasihi haufanywi kiholela, ila huzingatia vipengele fulani. Katika makala haya tumezingatia kipengele cha kisintaksia. Hiki ni kipengele kimojawapo kati ya vipengele vya kufanyia uchunguzi wa kimtindo vilichobainishwa na Leech na Short (2007) katika Orodha yao ya kategoria za kiisimu na kimtindo. Kwa mujibu wa Leech na Short, vigezo vya kileksika, kisarufi, tamathali za usemi na mshikamano na muktadha vinamsaidia mtafiti kukusanya data kwa mapana. Katika uchunguzi huu wa kimtindo wa riwaya ya *Paradiso* tunatumia kigezo cha kisintaksia katika kuchunguza suala la dini. Tunatumia kipengele hiki cha kisintaksia ndani ya Nadharia ya Uchimuzi iliyoasisiwa na wanaisimu wa Tapo la Prague katika karne ya ishirini. Tungo za kisintaksia tunazozichunguza ni zile zinazoibua maudhui kuhusu suala la dini. Habwe (2005) anaangazia kipengele cha dini katika riwaya yake kwa kuzingatia nafasi ya dini katika maisha ya kawaida ya wanajamii.

## Dhana za Mtindo na Usambamba

Kwa mujibu wa Kipacha na Jilala (2021), mtindo ni upangiliaji wa kazi unaohusisha mambo kama vile uchaguzi wa maneno, mpangilio wa sentensi na aya, na muonekano wa maandishi au mapigo ya sauti. Mtindo ni elementi muhimu sana katika kazi za kifasihi na ni wajibu wa mchanganuzi wa matini kuchunguza uteuzi wa msamiati, miundo na mipangilio ya sentensi, matumizi ya tamathali za usemi na sifa za uakifishi, dhamira, na mbinu nyinginezo (Wamitila 2008, kama anavyorejelewa na Kipacha na Jilala, 2021). Uhakiki wa kimtindo unaweza kubainisha sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi ya fasihi kama vile sifa za kifonolojia, kisintaksia, kimsamiati au kitamathali.

Orodha ya kategoria za kiisimu na kimtindo ya Leech na Short (2007) inabainisha vipengele vya kiisimu vinavyoweza kuzingatiwa kufanyia uchunguzi wa kimtindo. Miongoni mwa vipengele hivyo

ni leksimu, sarufi, tamathali za usemi, pamoja na muktadha na mshikamano. Katika uchunguzi huu tunazingatia kipengele cha kisarufi lakini tukitumia dhana mahsusi 'sintaksia'. Tukiongozwa na Nadharia ya Uchimuzi, tunazingatia kipengele cha kisintaksia cha usambamba, kama mhimili mmojawapo wa nadharia hii.

Kwa mujibu Wamitila (2003) usambamba ni mbinu ambapo msanii anayarudia maneno fulani au maana fulani kwa muundo mwingine tofauti. Pia, anasema kwamba urudiaji huu unaweza kuwa katika viwango tofauti kama vile vipashio vya kisintaksia – virai, vishazi, au sentensi. Jeffries na McIntyre (2010) wana mawazo yanayokaribiana na ya Wamitila. Wanaeleza kwamba usambamba unaweza kujitokeza katika viwango tofauti vya isimu: kisintaksia, kifonolojia na kisemantiki.

Mara nyingi mawazo hutolewa kwa njia ya sentensi. Usambamba unatusaidia kuchanganua kipashio cha sentensi kwa mujibu wa uchimuzi, ama tukizingatia kirai au kishazi ili kubaini maudhui ya mwandishi. Waandishi wa kazi za kifasihi husawiri maudhui katika kazi zao wakitumia ubunifu wa kiisimu kwa kuzingatia mbinu kama vile usambamba. Wasomaji hupata maudhui hayo kupitia kwa fasiri ya miundo ya kiisimu iliyotumiwa na mwandishi kusawiri maudhui hayo.

**Nduni za Kiusambamba Zilizotumika Kuibua Maudhui ya Dini katika *Paradiso***

Katika riwaya ya *Paradiso,* mbinu kadhaa za kiusambamba zimetumika katika kuibua maudhui kuhusu dini na mamlaka. Mbinu hizi ni pamoja na anafora, epifora, tanakuzi, mjalizo na uorodheshaji.

***Anafora***

Wamitila (2003) anaeleza kwamba anafora ni mbinu ya kibalagha au kiusemi ambayo inahusisha kurudia neno au kundi la maneno katika vishazi au sentensi zinazofuatana. Inawezekana kuiangalia anafora kama aina moja ya usambamba. Kwa mujibu wa Massamba (2004) kishazi ni tungo yenye kiima na kiarifu ambayo imo ndani ya tungo kuu. Tungo kuu inayorejelewa ni sentensi.

Lakini, kinyume na matarajio, vifungu vilivyorudiwa havileti uziada bali vinaimarisha ujumbe kwa njia ya msisitizo ambao unakumbukika na msomaji. Habwe (2005) ametumia mbinu hii katika riwaya yake *Paradiso*, kama tunavyoona katika madondoo mbalimbali kutoka katika riwaya hiyo.

1. [Michael] alitaka kuwa kama Yesu…**Hakuwa na** kwake. **Hakuwa na** gari. **Hakuwa** na mke. **Hakuwa na** nyumba.

(***Paradiso*, Ukur. 44**)

Katika dondoo la 1 tunaona kwamba mwandishi amerudiarudia kirai "**Hakuwa na"** ili kusisitiza ujumbe wake. Kirai ni kundi la maneno lisilokuwa na mahusiano ya kiimakiarifu (Massamba na wenzake 1999: 84). Katika dondoo la 1, kirai hicho "**hakuwa na"** kimerudiwarudiwa mwanzoni mwa kila kishazi. Lakini kirai kilichorudiwarudiwa kimefuatwa na kijalizo ambacho kinataja kitu ambacho Yesu hakuwa nacho. Badala ya mwandishi kuvitaja vitu ambavyo Yesu hakuwa navyo mfululizo katika orodha, anatumia mbibu ya anafora, ambapo kila faridi inajitokeza katika kishazi tofauti. Urudiaji huu unalenga kuipa uzito kila faridi ambayo ingekuwa katika orodha. Msisitizo huu wa kuiweka kila faridi katika kishazi tofauti unaifanya kila faridi iliyotajwa ikumbukwe kwa urahisi na msomaji.

Mwandishi analenga kusisitiza ujumbe kwamba si vizuri Wakristo kuwa na tamaa ya pesa na mali, kwa vile Kristo mwenyewe, ambaye ndiye msingi wa Ukristo, hakuwa na vitu vya dunia ambavyo wachungaji na Wakristo wengine wanavichukulia kama vitu vya muhimu zaidi kuliko kwenda paradiso. Mwandishi anaonyesha kwamba Yesu hakuwa na uwezo wowote wa kifedha wala mali, ingawa alikuwa na mamlaka kama mwana wa Mungu, na angaliweza kujipatia kila kitu kwa urahisi. Kama mhusika Michael anavyosema, kuwa mkristo ni kuwa kama Yesu. Hii inaashiria kwamba kuishi kama Yesu ni kuwa mfano kwa Wakristo wote. Katika kutumia anafora, mwandishi analenga kumulika suala la tamaa ya mali miongoni mwa wachungaji. Wachungaji wanahubiri injili ya utajiri, kinyume na mfano uliotolewa na Kristo mwenyewe. Hiki ni kinaya. Wachungaji ambao wanajiita Wakristo, na wengine hata wakiwa kwenye kiwango cha askofu wanashindwa kufuata nyayo za Kristo, ambaye ndiye kiongozi wa Kanisa.

Tamaa ya pesa na mali inajidhihirisha pia katika migogoro ndani ya makanisa. Migogoro hii inatokana na utashi wa madaraka na udhibiti wa zaka, pamoja na matoleo mbalimbali makanisani.

Kinyume na maelekezo ya Yesu kwamba kuwepo upendo kati ya waumini, kuna mifarakano na wivu ndani na kati ya makanisa, pamoja na wachungaji.

2. **Kundi la Michael** lilisisitiza kuna uhuru wa kukaa hali **kundi la** Joshua lilitaka liondoke. **Kundi la Joshua** lilidai kuwa ndilo lenye haki tu kuwepo katika jengo hili.

(***Paradiso*, Ukur. 76**)

Katika dondoo hili tunaelezwa kuwa badala ya kuwepo kanisa la pamoja, likiongozwa na Kristo mwenyewe, kuna migawanyiko ndani ya kanisa. Hata makanisa "yanamea" kila kukicha kwa sababu ya wachungaji kulenga na kushindania zaka na matoleo mbalimbali ya pesa kanisani. Makanisa yamekuwa kama biashara, yaani vyanzo vya kipato. Ushindani kwa ajili ya mamlaka katika makanisa umefungamana na tamaa ya pesa na mali. Kila mchungaji anataka amiliki kanisa lake ili akalidhibiti pamoja na kudhibiti mapato ya kanisa hilo. Badala ya wachungaji kushindania kuihubiri injili ya Bwana, wao wanashindania mali na pesa. Mali na pesa ni vitu vya paradiso ya hapa duniani, siyo paradiso ya baadaye. Hii ni kweli kinzani kwa vile kusudi la Mkristo yeyote ni kwenda paradiso ya baadaye. Wachungaji Michael na Askofu Joshua wanashindania uongozi wa kanisa la New Jerusalem. Badala ya kuwepo undugu kati yao unaosisitizwa na Kristo, kuna uhasama. Wachungaji wanashindwa kuafikiana kama ndugu katika Kristo. Mwandishi anaonyesha kwamba wachungaji (na hata kanisa kwa jumla), wameshindwa kuwa kielelezo cha undugu kwa jamii. Hiki ni kinaya. Ni kinaya kwamba wahubiri wameshindwa kuendeleza upendo wanaouhubiri. Pia ni kinaya kwamba wachungaji ambao wangekuwa msitari wa mbele katika juhudi za kwenda paradiso ya baadaye ndio wanaoshindania paradiso ya hapa duniani.

Zaidi ya kushindania zaka na matoleo mbalimbali kanisani, wachungaji wanaonyesha tamaa ya pesa na mali kwa njia ya ulanguzi wa madawa. Mwandishi tena ametumia mbinu ya anafora kuangazia tatizo hili (ulanguzi wa madawa) linaloyaathiri maeneo ya miji. Anaonyesha jinsi ambavyo ulanguzi wa madawa ni tatizo jijini Nairobi na Kenya kwa jumla.

3. **Waumini wengine** walipofanya bidii katika sala **wengine** wakalangua madawa. Waumini **wengine** walipoufuata uso wa Bwana, wenzao **wengine** waliuza bangi katika mataifa ya nje ili kupata dola.

(***Paradiso*, Ukur. 208**)

Katika dondoo la 3, tunapata sentensi mbili changamani zenye vishazi huru na vishazi vitegemezi. Sentensi zote mbili zinaanza na kirai "waumini wengine", ila vishazi huru katika sentensi hizi vinaanza na maneno 'wengine' na 'wenzao' ambayo yanatenda kama viwakilishi kwa vile mwandishi asingetumia nomino 'waumini' mwanzoni mwa kila kishazi. Kutumia nomino 'waumini' mwanzoni mwa kila kishazi katika sentensi hizo mbili changamani kungemchosha msomaji. Hii ingekuwa kinyume na lengo la mwandishi la kuivuta nadhari ya msomaji ili aweze kufikia ujumbe lengwa. Kwa hivyo, nomino kiima 'waumini' imedondoshwa mwanzoni mwa vishazi huru, ila imeashiriwa kwa matumizi ya kiwakilishi 'wengine.' Ingawa neno 'wengine' limerudiwa mara nne, urudiaji wake hauchoshi kwa vile mwandishi ametumia nomino 'waumini' mwanzoni mwa sentensi hizo mbili. Urudiaji wa kiwakilishi 'wengine' cha nomino 'waumini' kama sehemu ya kiima mwanzoni wa kila kishazi unalenga kusisitiza mlinganuo kati ya matendo yanayofaa na yale yasiyofaa. Ili kuyachimuza matendo yasiyofaa, mwandishi ameyaweka katika vishazi huru ambavyo vinajitokeza baada ya vishazi vitegemezi. Hii ni kwa sababu faridi ambazo zimetajwa mwishoni mwa sentensi ndizo zinazokumbukika zaidi akilini mwa msomaji. Kwa hivyo, Habwe (2005), akitumia mbinu ya anafora, ameweza kuyamulika matendo ya ulanguzi wa madawa na uuzaji bangi ambayo yanaiathiri jamii. Tatizo la ulanguzi wa madawa kujitokeza ndani ya kanisa ni kinaya kwa vile kanisa ndilo linalofaa kukikemea kitendo hicho.

***Epifora***

Tofauti na urudiaji wa kianafora ambao unatokea mwanzoni mwa vishazi au sentensi, urudiaji wa kiepifora unatokea mwishoni mwa vishazi au sentensi zinazofuatana. Habwe (2005) ameitumia mbinu hii pia katika riwaya yake ya *Paradiso* kuibua maudhui ya uaminifu katika ndoa.

4. Kwa kweli vitendo vya mzazi huwa mfano mwema kwa wana. Yeye Joshua **hakuwa mwaminifu**. Wala Lona **hakuwa mwaminifu**.

(***Paradiso*, Ukur. 129**)

Katika dondoo hili tunaona jinsi ambavyo watu wanaochukuliwa kuwa ni mfano wa mienendo inayofaa katika jamii (yaani wachungaji) wameshindwa kutekeleza dhima hiyo. Wachungaji, kinyume na matarajio ya wanajamii, sio waminifu katika ndoa zao. Mwandishi ametoa mfano wa Askofu Joshua na mkewe Lona ili kudhihirisha maudhui haya. Wachungaji hawa wote wawili (mume na mke) wanahusika katika mapenzi nje ya ndoa. Hili ni jambo ambalo limesisitizwa kwa urudiaji wa kiarifu kile kile (hakuwa mwaminifu) katika sentensi mbili zinazofuatana. Pia, badala ya kutumia sentensi moja kwa kusema Joshua na Lona au Joshua na mkewe hawakuwa waminifu, mwandishi anamwelezea kila mhusika kivyake, yaani kila mhusika ni kiima katika sentensi kinachoelezwa kwa kiarifu, badala ya wahusika hao kuunda kiima kimoja na kuelezwa kwa kiarifu kimoja. Kwa kuwaelezea wahusika hawa katika sentensi mbili, mwandishi anachimuza ile taarifa kuu inayowahusu, yaani anasisitiza kwamba kila mchungaji (Joshua na Lona) hakuwa mwaminifu katika ndoa. Kwa kutumia mbinu ya epifora, mwandishi anammulika kila mhusika kivyake ili msomaji azingatie mwenendo huu miongoni mwa wachungaji na katika kanisa kwa jumla. Mwandishi anaonyesha kwamba kuna shida kubwa katika kanisa na jamii kwa jumla.

***Tanakuzi***

Mbali na mbinu za anafora na epifora, matumizi ya mbinu ya tanakuzi nayo yanadhihirika katika riwaya ya *Paradiso*, mintarafu usawiri wa maudhui ya dini. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), tanakuzi inarejelea misemo inayoelekea kupingana na kuwa na maana tofauti. Ni mbinu inayoyaweka sambamba maneno au mawazo kinyume. Mlinganuo kati ya maneno au mawazo husika hupelekea msisitizo fulani na huashiria ujumbe wa mwandishi. Michira (2018) anasema kuwa tanakuzi ni mbinu ya kuyaweka kwa makusudi maneno, miundo ya kisarufi (virai, vishazi au sentensi) au mawazo kinyume ili kuonyesha au kusisitiza hitilafu za asili katika maisha. Tanakuzi inapotumika kiusambamba, kuna ruwaza ya kujirudia, lakini sehemu zinazojirudia zinakinzana au huwa ni vinyume.

Habwe (2005) ameitumia tanakuzi kuipiga vita tabia ya tamaa katika jamii. Anaonyesha kwamba tamaa ya mali na pesa haina maana yoyote. Mwishowe, tamaa ya vitu vya dunia inaleta majuto na kukata tamaa.

5. Nyumba hii Boribori ameihama sasa. **Hakuihama** kwa hiari, **amehama** kwa lazima. **Amehama kwa ajili ya hadaa**. Sasa Boribori analala mto uliochanika.

(***Paradiso*, Ukur. 222**)

Katika dondoo la 5 tunaonyeshwa hali ambapo mchungaji Boribori yuko jelani kwa kulangua madawa. Badala ya kuishi maisha mazuri katika nyumba yake ya kifahari, sasa amehamia mahali ambapo hali ni tofauti kabisa na ile katika nyumba yake. Sehemu za muundo wa usambamba wa kitanakuzi ni "amehama…. Hakuihama." Kila kishazi katika dondoo la 5 kina ujumbe wake. Kwanza tunaambiwa kwamba Boribori amehama. Kisha tunaambiwa mazingira ya kuhama kwake, yaani sio kwa hiari bali kwa kulazimika. Amehama kwa ajili ya hadaa zake. Mbinu ya tanakuzi imetumika kwa njia ya kuweka kishazi kikanushi kinachoonyesha hali asiyoitaka Boribori kikifuatwa na kishazi kinachotaja kwamba hakuweza kuyadhibiti yaliyotokea kutokana na vitendo vyake. Tunapochunguza dondoo hilo tunaona kwamba mwandishi, kwanza kabisa ametaja hali ambayo imejitokeza kumhusu Boribori. Kisha anatuambia kwamba mhusika hakuitaka hali hiyo. Baadaye, katika kishazi cha tatu mwandishi anatuambia kuwa msingi wa kuhama kwake ni hadaa zake. Kwa kutumia mbinu ya tanakuzi, mwandishi anaonyesha athari za Mkristo kufanya yasiyofaa. Boribori ni mfano kwa wachungaji wengine na tena Wakristo kwa jumla wanaojihusisha na mbinu za kutafuta utajiri kwa njia yoyote ile.

***Mjalizo***

Mjalizo ni mbinu nyingine ya kisintaksia iliyotumiwa na Habwe (2005) katika riwaya yake ya *Paradiso* kusawiri maudhui ya dini. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) mjalizo ni mbinu ya kibalagha ambapo maneno au virai vinawekwa pamoja bila ya matumizi ya viunganishi kwa sababu za ikitisadi

ya maneno na kuzua kasi fulani inayohitajika. Ingawa Mbatiah (2001) anatumia istilahi 'asindeto' inayotokana na utohozi wa neno la Kiingereza *asyndeton*, anaonyesha kwamba mbinu hii inaweza pia kuitwa 'mjalizo.' Anaeleza kuwa asindeto ni kunga ya mtunzi ambapo viunganishi hudondoshwa katika tamko ili kuleta wekevu na kasi ya masimulizi au maelezo. Tena, anasema kwamba mbinu hii inatumiwa kuleta ridhimu katika maandishi.

Mbinu ya mjalizo inatumiwa kukifanya kirai au sentensi kuwa fupi na kusomeka kwa kasi. Kwa mfano, mwandishi anaweza akaacha kutumia kiunganishi 'na' kabla ya faridi ya mwisho katika mlolongo wa virai au vishazi ili kuboresha mtiririko na usahili. Mbinu hii imetumika katika riwaya ya *Paradiso* kuonyesha hali ya msambaratiko katika kanisa.

**6.** [Michael] aliona kanisa la Bwana likisambaratika **kila siku**, **kila mwezi**, **kila mwaka**.
(***Paradiso*, Ukur. 77**)

Katika dondoo la 6 mwandishi ametumia mbinu ya mjalizo kwa kudondosha kiunganishi baina ya virai viwili vya mwisho kwenye mlolongo wa virai ambavyo vingeunganishwa kwa kiunganishi. Yaani, badala ya kusema "**kila siku, kila mwezi *na* kila mwaka"** mwandishi anasema "**kila siku, kila mwezi, kila mwaka."** Mwandishi amefanya hivi ili kujenga ridhimu na msisitizo fulani kuhusu suala la mgawanyiko katika kanisa. Wakati msomaji akisoma tungo hiyo, anafuatanisha virai hivyo akilini mwake. Ridhimu hiyo inakaa akilini mwake, tena na jambo linalozungumziwa na mwandishi, yaani kusambaratika kwa kanisa la Bwana. Hata virai vinavyojenga mjalizo katika dondoo hilo vinadhihirisha mgeuko wa polepole ambapo mwandishi anaonyesha kiasi cha mgawanyiko kwenye kanisa, yaani kuanzia kwa kipindi kifupi cha siku hadi kipindi kirefu cha mwaka.

Kulingana na mchungaji Michael, migogoro kanisani inatokana na ushindani kanisani kwa ajili ya vitu vya dunia. Ushindani huu unatokana na ulafi na tamaa ya vitu hivi.

**7.** Kisa na maana ni nini?" Michael aliwaza. **Ushindani**, **ulafi** wa vitu vya dunia hii. **Tamaa** ambayo Bwana Yesu alisema tusiwe nayo.
(***Paradiso*, Ukur. 77**)

Katika kuelezea hali ya tamaa na ushindani, mwandishi anafuatanisha faridi mbili 'ushindani' na 'ulafi wa vitu vya dunia' bila kiunganishi 'na' ambacho kwa kawaida huwekwa kati ya faridi mbili zilizoorodheshwa. Mwandishi anataja faridi mbili, halafu anaweka kituo mwishoni mwa faridi hizo kama kwamba tungo yenye faridi hizo ni sentensi, yaani: "**Ushindani**, **ulafi** wa vitu vya dunia hii." Nomino hizi mbili (ushindani na ulafi) zingeunda kirai nomino kimoja, yaani 'ushindani na ulafi'. Lakini, badala ya kufanya hivyo, mwandishi amezichimuza nomino hizo kwa kutumia mbinu ya mjalizo, yaani kutokiweka kiungaanishi 'na' kati ya nomino hizo. Kwa vile tungo hiyo yenye mjalizo haina kiarifu, kimuundo si sentensi. Tungo inayofuata tungo hiyo ni kishazi kitegemezi ambacho pia kimewekewa kituo kama kwamba ni sentensi. Kishazi hiki kingeambatanishwa na kishazi cha awali kwa alama ya kistari kirefu kwa vile kinaendeleza maudhuhi ya ulafi. Lakini badala ya kufanya hivyo mwandishi anakifanya kishazi hicho kitegemezi kisimame kama sentensi. Hata hivyo, tungo ambazo hazikukamilika kama sentensi kimuundo ni za kawaida katika kazi za kifasihi. Ni njia ya usisitizaji. Tungo hizi ambazo hazikukamilika kama sentensi (kwa mujibu wa sentensi kuwa na muundo wa kiima na kiarifu) zinaakisi maudhui ya msambaratiko katika kanisa. Kishazi kitegemezi kinachoanza na neno "tamaa" kinahitimisha yale ambayo mwandishi ameyazungumzia katika kishazi cha awali. Mwandishi ameyachimuza maudhui ya tamaa kwa kukifanya kishazi hiki kisimame kama sentensi. Maudhui ya tamaa yamesisitizwa sana katika riwaya hii.

***Uorodheshaji***

Katika kusawiri maudhui ya dini katika riwaya yake ya *Paradiso*, Habwe (2005) pia ametumia mbinu ya kisintaksia ya uorodheshaji. Kulingana na Galperin (1977), uorodheshaji ni mbinu ya kimtindo ambapo vitu, fenomena au sifa hutajwa kwa mfuatano ili kuzalisha mfululizo wa vitu vya jinsi moja kisemantiki, hata kama uhusiano wa kisemantiki kati ya faridi zilizo katika mfululizo ni wa mbali. Anaeleza kwamba uorodheshaji unaashiria uhusiano kati ya faridi zilizotajwa katika mfufulizo. Katika uorodheshaji, maneno, virai, au vishazi vinaorodheshwa kwa mfululizo katika sentensi au aya. Lengo la uorodheshaji huwa ni kuzichimuza faridi zilizoorodheshwa.

Habwe (2005) ametumia mbinu hii ya uorodheshaji kusisitiza motifu ya tamaa katika *Paradiso*. Kama tulivyoona awali (dondoo la 5), tamaa ni chanzo cha vitendo mbalimbali visivyofaa katika jamii, kama vile ulanguzi wa madawa.

**8.** Vitendo vya dini vilimuudhi. Kelele na vurumai vilishtadi kanisani. Huko walitafuta pepo lakini huko ndiko walikokugeuza na kukufanya Jehanamu kwa **vitendo, tamaa na utashi wa dunia**.

(***Paradiso*, Ukur. 97**)

Mhusika anayezungumziwa katika dondoo la 8 ni Lydia. Kupitia kwa mawazo ya mhusika huyu, pamoja na mbinu ya uorodheshaji, mwandishi anaonyesha vitendo visivyofaa ambavyo vinaliathiri kanisa. Mwandishi ameorodhesha vitendo, tamaa na utashi wa dunia kama tabia ambazo zinalikumba kanisa. Tabia hizi haziambatani na mwenendo wa Kikristo. Tabia hizo zimetajwa kiusambamba kwa orodha: **vitendo, tamaa na utashi wa dunia.** Maudhui ya tamaa ndani ya kanisa yamewasilishwa pia kwa njia ya mjalizo (dondoo la 7) ambapo mchungaji Michael anakemea "**ushindani**, **ulafi** wa vitu vya dunia hii. **Tamaa…**" Kwa vile vitendo hivi vimekemewa katika sehemu mbalimbali za riwaya ya *Paradiso*, tunaona kwamba mwandishi wa riwaya hii anaiangalia tamaa kama tatizo kubwa katika jamii. Mwandishi anatuambia kwamba kuna shida kanisani, na katika jamii kwa jumla, kwa vile tamaa ni msingi wa vitendo vingi visivyofaa katika jamii.

***Mdafao wa Urudiaji***

Katika kuchunguza matumizi ya usambamba katika riwaya kama nduni ya kimtindo, tunaweza pia kuangalia mdafao wa urudiaji wa vifungu, ambao unaashiria kiasi cha msisitizo wa ujumbe wa mwandishi. Mwandishi anarudiarudia miundo ya lugha kulingana na dhamira yake. Akitaka kulisisitiza zaidi jambo fulani anarudia vifungu mara nyingi zaidi. Miundo inayofanana ndiyo inayojirudia. Miundo inayojirudia huwa ina ujumbe unaolingana na ambao ndio unaosisitizwa. Katika *Paradiso*, tunaona kwamba urudiaji wa vishazi kiusambamba unatokea mara mbili hadi mara tano.

*Mdafao wa Usambamba wa Urudiaji wa Vishazi*

*Usambamba wa Urudiaji Mara Tano*

**9.** Nyinyi ni shetani. Ati wahubiri? Wahubiri gani nyinyi? Nyinyi ni laghai. **Mwaiba**. **Mwalazimisha**. **Mwaongopa**. **Mwaua**. Huku **mwataja Yesu**. Shetani wakubwa nyinyi. Msitaje jina la Bwana bure.

(***Paradiso*, Ukur. 75**)

Katika dondoo la 9, tunaona urudiaji mara tano wa vishazi. Urudiaji sio wa kiujumi tu, bali unalenga kuangazia tabia za baadhi ya wachungaji. Mwandishi, kupitia kwa mhusika Musa, anatujulisha kwamba tabia hizo mbovu zimo kanisani, jambo ambalo ni kinaya, kwa vile injili ya kikristo inakemea vitendo hivyo vilivyotajwa na Musa. Vitendo vinavyodhihirika kanisani vinatajwa katika sentensi fupi fupi za kishazi cha neno moja moja, isipokuwa kishazi cha tano, ambacho kimetanguliwa na kielezi 'huku.' Kusudi la mwandishi la kuvitaja vitendo vya wachungaji kwa sentensi fupifupi za kishazi kimoja kimoja, badala ya kuvitaja katika orodha, vikitenganishwa na alama ya mkato ni kukisisitiza kila kitendo kwa kukipa uzito zaidi. Kwa kutumia njia hii, mwandishi anakifanya kila kitendo kidhihirike zaidi akilini mwa msomaji. Inamwezesha mwandishi kufikisha ujumbe wake kwa msomaji. Musa anafichua unafiki wa Askofu Joshua na mke wake Lona. Kwa sababu ya unafiki wanalitaja jina la Bwana bure.

Lakini kwa kuwa sentensi huwa na muundo wa kiima na kiarifu tunaona kwamba katika vishazi ambavyo vimesimama kimoja kimoja kama sentensi, nomino kiima 'Joshua na Lona' (ambayo imewakilishwa na kiwakilishi 'nyinyi,' ambacho pia kimedondoshwa katika muundo wa nje), imeakisiwa katika tungo tenzi kwa kipatanishi 'mw-.' Kishazi cha tano kina muundo tofauti kidogo na ni kama hitimisho la vitendo vilivyotajwa awali, yaani kwamba Askofu Musa na mke wake Lona wanafanya yale ambayo amekwishayataja (katika vishazi vinne vilivyotangulia) huku wakitaja Yesu. Kishazi hicho cha mwisho kinafanya kazi kama kielezi cha vishazi vilivyotangulia na kinabainisha unafiki wa wachungaji.

*Usambamba wa Urudiaji Mara Nne*

Urudiaji mara nne tunaushuhudia katika dondoo la 1 ambalo tumekwishachambua maudhui yake. Hapa tunalirejelea kwa kigezo cha wa idadi ya marudio ya virai au ya vishazi:

**10.**[Michael] alitaka kuwa kama Yesu… **Hakuwa na kwake**. **Hakuwa na gari**. **Hakuwa na mke**. **Hakuwa na nyumba**.

(***Paradiso*, Ukur. 44**)

Katika dondoo hili tunapata urudiaji wa kianafora mara nne. Vishazi vyote vilivyorudiwa vina muundo sawa. Tofauti iko katika nomino kijalizo peke yake. Badala ya kutumia alama ya mkato kutenganisha vitu ambavyo Yesu hakuwa navyo, yaani akasema, "Yesu hakuwa na kwake, gari, mke na nyumba," mwandishi anavitaja vitu ambavyo Yesu hakuwa navyo akitumia vishazi huru vinne ambavyo vinafanana kumuundo. Urudiaji huu mara nne unasisitiza maudhui kwamba Mkristo anafaa kutokuwa na utashi wa vitu vya dunia, yaani kwa kuuiga mfano wa Yesu.

*Usambamba wa Urudiaji Mara Tatu*

Urudiaji mara tatu nao unadhihirika katika riwaya ya *Paradiso* kama tunavyoona katika dondoo lifuatalo:

**11.**Ni wangapi walao rushwa? Ni wangapi wauao? Ni wangapi wadanganyao?"

(***Paradiso*, Ukur. 130**)

Katika dondoo la 11 tunapata mawazo ya mchungaji Lona. Lona anajaribu kuhalalisha vitendo vyake visivyo vya kimaadili ambavyo yeye mwenyewe anaona havitamwezesha kwenda paradiso. Lakini Lona anaona kwamba madhali hayuko peke yake katika kufanya vitendo hivyo ambavyo yeye mwenyewe anajua kuwa ni dhambi, haina shida. Anaona kwamba Labda atasamehewa pamoja na watu wengine watendao vitendo hivyo. Katika urudiaji huo mara tatu, mwandishi ametaja vitendo vitatu ambavyo havifai kwa mtu anayejiita Mkristo. Anatumia urudiaji mara tatu kuvimulika vitendo hatari katika jamii, yaani rushwa, mauaji na udanganyifu.

*Usambamba wa Urudiaji Mara Mbili*

Urudiaji mara mbili umetumika kuwasilishia maudhui ya malalamiko kuhusu makanisa ya kiprotestanti. Baadhi ya wanajamii wanakerwa na jinsi ibada za makanisa ya kiprotestanti zinavyoendeshwa. Lakini kinachowakera hasa ni unafiki wa waumini ambao hawatekelezi mafunzo yanayowapeleka kanisani.

**12.**Vitendo vya dini vilimuudhi. Kelele na vurumai vilishtadi kanisani.

(***Paradiso*, Ukur. 97**)

Katika dondoo la 12 tunamwona mhusika Kyalo akionyesha kukerwa na vitendo vya dini. Mawazo yake yamerudiwa katika vishazi viwili vinavyolingana kimuundo. Kishazi cha kwanza kinataja kukerwa kwake. Kishazi cha pili kinataja vitu vinavyomkera hasa, yaani kelele na vurumai kanisani. Muktadha wa mawazo ya Kyalo ni kwamba waumini wanafanya kelele na vurumai kanisani wakati ambapo wana tamaa na utashi wa vitu vya dunia. Hiyo ndiyo tabia ya waumini inayomkera hasa. Mwandishi amemtumia mhusika huyu Kyalo kudhihirisha kinaya hicho.

**Hitimisho**

Kutokana na uchunguzi huu tunaona kwamba Habwe (2005) ametumia nduni mbalimbali za usambamba kimtindo ili kuibua maudhui ya dini katika riwaya yake ya *Paradiso*. Miundo ya kiusambamba iliyotumika ni pamoja na anafora, epifora, tanakuzi, mjalizo na uorodheshaji. Kwa vile usambamba unahusisha urudiaji, makala haya yamefafanua mdafao wa urudiaji unaohusika. Hii ni kwa sababu mdafao wa urudiaji unaathiri kiasi cha msisitizo. Unaonyesha hisia za mwandishi na masuala anayoyachukulia kuwa ni ya muhimu zaidi. Inabidi msomaji achunguze miundo iliyotumiwa na mwandishi ili kufikia fasiri ya miundo hiyo, yaani sababu inayopelekea kutumika kwa miundo husika katika kazi ya kifasihi. Kwa kufanya hivyo, ataweza kufikia ujumbe na maudhui ya mwandishi. Mwandishi anatunga kazi ya kifasihi, lakini kazi hiyo haikamiliki mpaka msomaji anapoisoma na kufasiri yaliyomo. Mwandishi huyawasilisha yaliyomo akitumia mbinu mbalimbali za

kiisimu, mkiwemo mbinu za kisintaksia. Katika kuifasiri kazi ya kifasihi, msomaji huijenga tena akilini kazi hiyo, kwa vile hana maelezo ya moja kwa moja kutoka kwa mwandishi.

**Marejeleo**

Galperin, I. R. (1977). *Stylistics* (2nd Ed.) Moscow: Vishaya Shkola.

Habwe, J. (2005). *Paradiso*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Jeffries, L. & McIntyre (2010). *Stylistics.* United Kingdom: Cambridge University Press.

Kazungu, K. (1982). *Deviation and Foregrounding in Chosen Literary Texts* [Unpublished Master's dissertation]. University of Nairobi.

Kipacha, A., & Jilala, H. (2021). *Nadharia za Elimumitindo ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Daud Publishing Company Ltd.

Kitsao, J. (1975). *A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts* (Unpublished Master's Dissertation). University of Nairobi.

Kitsao, J. (1982). *An Investigation of Themes in Swahili Literature and An Application of Stylostatistics to Chosen Texts*. Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Leech, G., & Short, M. (2007). *Style in Fiction* (2nd Ed.). United Kingdom: Pearson Education Limited.

Massamba, D. P. B., *et al*., (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks, Graphics and Publishing.

Michira, J. N. (2018). A Stylistic Analysis of John Habwe's Pendo la Karaha. *International Journal of Humanities and Social Sciences, 6*(6).

Short, M. (2013). *Exploring the Language of Poems, Plays and Prose.* New York: Routledge.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.